# TAMATHALI ZA SEMI ZA KISWAHILI*

*Muhammed Seif Khatibu*

## Utangulizi

Mgodi wa Fasihi ya Kiswahili hasa katika tanzu hai ya tamathali za semi ni dafina kubwa isiyoweza kuchimbwa na kumalizika. Utajiri huo mkubwa uliojilimbikiza katika tanzu zote za fasihi ni ushahidi usiopingika juu ya ukuu wa fasihi ya Kiswahili na uhai wake. Si fasihi andishi wala sio ile simulizi itolewayo ana kwa ana itakayokosa jicho la msomaji wa fasihi kukosa kukwaa tamathali tosha. Si riwaya, ndefu au fupi, iliyofinyangwa kiriwaya na kufuata miiko na kunga zake zinazosadifu, itakayobeza umuhimu wa tamathali hizi. Aidha, si shairi si tenzi, wala nyimbo iliyofinyangwa na kusukwa vilivyo itakayoweza kukengeuka angalau ukufiwa semi. Nazo tamathiliya zimeshehenezwa semi tumbitumbi ili ziweze kuteka masikizi na maoni ya watazamaji au wasikilizaji. Semi hizi ndizo zinazoipa hadhi na heshima sio fasihi ya Kiswahili tu katika fani yake bali pia zinaifungua uso lugha yenyewe na kuwapa ariha watunzi kutunga kile wakipendacho kwa kifua mbele.

Makala hii itajikusuru kuchota "*gao*" tu la tamathali za semi. Aidha, makala haitajifunga na tanzu maalumu bali itaranda kuchota semi hizi hapa na pale. Tamathali hizi hutumika katika mazingira halisi ya Waswahili. Hazitoki katika ombwe au kutotolewa kama vifaranga vya kuku. Hubuniwa na kutumika katika shughuli za kila siku za maisha ya watu. Kwa mfano, katika kilio na misiba, katika maziko na matanga, tamathali hutumika kuliwaza wafiwa na wenye misiba. Katika mizungu na kunga za kuwafunda wari - mangariba, makungwi na manyakanga huwa na uwanja wao wa kuzitumia semi zenye mnasaba na mazingira yao. Ingia gulioni au wengine huita sokoni au "*marikiti*" - utashughudia semi zinazofyatuliwa humokutoka midomoni mwa madalali, wachuuzi, wanunuzi na hata wachukuzi. Nafasika na uruhusike katika pungo za pepo na mashetani uone muwele anapopandisha pepo kichwani huku semi kadhaa zikitumika kupandisha madadi yake. Hii inadhihirisha kuwa semi hizi zinaambatana naamali na kazi za Waswahili katika maisha yao ya kila siku.

Tamathali za semi ni nini? Kwa mujibu wa Mulokozi na Kahigi (1979), Tamathali za usemi ni vifananisho au viwakilisho vya dhana fulani kwa dhana nyingine tofauti au zinazofanana. Ni usemi wenye kupanua, kupuuza au kubadilisha maana za dhahiri au za kawaida za maneno ili kuleta maana maalumu iliyokusudiwa na mtunzi au mzungumzaji. Tamathali nzuri huyakinisha na kuipa uhai na uhalisi zaidi dhana inayoelezwa, huburudisha na kuzindua akili ya msomaji au msikilizaji na kuacha athari ya kudumu katika hisi na mawazo yake.

* Makala hii ilitolewa kwa mara ya kwanza katika MULIKA 18.

Utamu wa lugha haupo tu katika maudhui yaani kile kinachoelezwa - bali pia ladha ya lugha huzidi kwa ustadi wa kuyaelezea maudhui yenyewe. Makala hii haitashughulikia kile kinachozungumzwa bali namna kinavyozungumzwa na mvuto upatikanao. Sitazichambua semi zote ziliomo katika lugha hii kwa sababu tatu muhimu. Mosi, sizitambui semi zote za Kiswahili zilizopo. Pili, lugha ikiwa kitu chenye uhai kiwezacho kufa kama kilivyokufa Kilatini au kiwezacho kukua kama Kiswahili kinavyozidi kupata heshima na hadhi yake duniani, lazima itazalisha semi kadha wa kadha siku hadi siku. Kwa hivyo ziko semi zisizotumika kabisa katika Kiswahili na zipo zinazoibuka siku hadi siku. Na tatu sio nia yangu kabisa kuandika kila semi niijuayo au niambiwayo. Nianze na tashbiha.

**Tashbiha**

Huu ni usemi unaolinganisha vitu viwili halisi vinavyoonekana ambavyo vinaleta mshabaha. Katika tashbiha maneno kama mithili au *kwamba* hutumiwa kufananisha vitu viwili. Katika mifano ifuatayo ya nyimbo, shairi, methali, na riwaya, tashbiha zipo tele.

Kwa mfano, katika nyimbo ya taarabu mwimbaji anamsikitikia mpenzi wake kuwa kwa ajili ya mapenzi yao na kwa kuwa hamuoni, pendo hili limemtibua maradhi ya kukondeana na sasa anaonekana mwembamba mfanowe uzi. Ndwele hiyo inashabihishwa hivi:

Mimi naumwa mpenzi, Uko wapi muhisani
Nimekonda kama uzi, Hali yangu huidhani
Zanidhofisha simanzi, niwasiliye fulani.

Tukimwacha muwele anayekonda kama uzi na tumwangaliye "nyakanga" wa mashairi ya Kiswahili Marehemu Shaaban Robert wakati wa ujana wake anavyomsifu mpenzi wake kwa vile anavyoweza kumlewesha na kumpumbaza kwa ufundi wake wa kumpa mahaba pale anavyotongoa. Kutoka kitabu cha *Mwafrika Aimba*, Shaaban atongoa hivi:

Ukimshika mahali, huruka *kama mkizi*
Utajua kwa dalili, kama kaazimu kazi
Hulainisha mwili, *kama samli ya mbuzi*
Mahaba ya mjakazi, sijaona mfanowe (Uk. 37)

Na katika methali za Kiswahili mifano miwili hii inatosha, kutoa uzito kwa dhima nzima hii;

Jambo usilolijua *kama* usiku wa kiza
Kawaida ni kama *sheria*

Katika riwaya ya *Nyota ya Rehema* tutachota vifungu viwili vinavyodhihirisha hali hiyo ya kitashbiha.

Mwandishi aliandika hivi katika ukurasa wa riwaya hii, "Fuadi alimpokea Aziza kama mtoto apokeavyo zawadi..."

Na katika riwaya ya *Utengano* ya Said Ahmed Muhammed, inaonekana inapolinganishwa weusi wa jongoo na weusi wa muhusika bwana Haji, pale ilipoandikwa, "Bwana Haji alisitawi kwa ule weusi wake wa kama jongoo..." (Uk. 104).

Tashbiha hiyo pia inachorwa katika riwaya maarufu ya Muhammed Saidi Abdulla, riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*. Mwandishi anauelezea kitashbiha;

"Bwana Msa" alichungulia tena. Ndani mlikuwa na kiza *kama uwanda wa ahera*. Kiza kilikuwa kimetapakaa, kinavuja!

**Sitiari**

Ni aina nyingine ya tamathali ya semi. Sitiari hutokea kitu kinapopewa jina la kitu kingine. Uhamishaji huu huwa kutoka kwenye aina moja ya vitu au kwa mujibu wa kufanana kwa vitu hivyo. Katika nyimbo hii ya taarabu inayoonyesha hali ya udhalimu, uonevu na ukandamizaji kwa jamii ya Zanzibar kabla ya Mapinduzi ya 1964, yaonyesha makandamizo hayo sawa na pazia zito lililougubika umma wa Zanzibar na kunyonya damu yao.

*Pazia lile la giza*, Lilotuweka gizani
Damu yetu likifyonza, Wanyonge ndani kwa ndani.

Methali za Kiswahili pia zina shehena nzima za semi za aina hii, methali hizi tatu zitatosha kutia uzito wa hoja hiyo.

1. Mgeni ni kuku mweupe
2. Mke ni nguo, mgomba kupaliliwa
3. Kufa kikondoo, ndiko kufa kiungwana

Na katika riwaya za Kiswahili, *Utengano* (Uk.23) inasema, "... *radhi za wazee ni fimbo kubwa* ukizikosa".

Shaaban Robert katika *Kusadikika* (uk. 1) anasema "...Baba yake alipokuwa *nahodha wa chombo* cha serikali yeye alikuwa *rubani* wake, akenda katika hali hiyo mpaka wakati wa enzi ya mfalme mpya..."

**Tashihishi**

Huu ni usemi unaotumiwa kwa vitu vile ambayo havina uhai wala tabia za mwanadamu lakini vinapewa uhai na sifa zote za mwanadamu. Kitu ambacho kwa maumbile yake hakitembei, hakisemi hakizai wala kufa, hupewa uwezo wa yote hayo katika fani ya fasihi.

Mshairi wa taarabu analilalamikia pendo lake linalomuadhibu. Analalama hivi, kama vile eti litamsikia na kupumzisha:

Kulibeba nimechoka, Pendo nilifanye nini?
Halitaki kunishuka, Limenikaa moyoni
Nataka kupumzika, Laumiza kifuani.

Na katika fani ya vitendawili tashihishi haijifichi. Hapa popoo zinapewa uwezo wa kuvuka mto na huku kivuli kupewa uwezo wa kutembea.

1. Popoo mbili zavuka mto (Macho)
2. Popote niendapo anifuata (Kivuli)

Na katika methali "kiburi" inapewa sifa za ubinadamu ya kuwa mwungwana pale aliposema.

Kiburi si mwungwana.

Au pia pale mtungi na kata vitu vya kuhifadhia na kunywea maji ambavyo havina uhai vinapotakiwa viulizane,

Siri ya mtungi muulize kata.

Katika Utengano (Uk. 23) Simango inapewa uwezo wa kudadisi moyo:

"Moyoni mwake mlikuwa na *simango lilomdadisi*
kwa nini mpaka leo hajakata pingu za utumwa".

Muhammed Suleiman katika *Nyota ya Rehema* (Uk. 5) anayapa maua na miti ya fito iliyoko katika kitalu hali ya ubinadamu kwa kusema,

"... Tena fito za kijani za minarigisi *zilisimama cheni* katika magudulia ya nakshi, kila kichwa cha minarigisi kimeeleka ua zuri jeupe, na *mafumbu yaliyokaa tayari* kuendeleza haiba ya ukoo wake. Baadaye ilifuatia miwaridi, miasumini, mikilua, na hata mihanuni...".

Tashihishi pia inatoa haiba pale matawi ya miti yanapopewa uwezo wa kibinadamu wa kuweza "kukaba roho" na kuua. Riwaya ya *Nyota ya Rehema* inadhihirisha hivi; "Matawi makaidi yalichomoza kati yake mfano wa mikono iliyotega *kukaba roho za wapitao*".

Na riwaya hiyo hiyo tunaelezwa kuwa mashuke ya mpunga yakisali kwa kusujudu;

"... Mashuke ya mpunga yalitikisa vichwa kwa umoja, yakasujudu..."

Na katika tungo maarufu ya tenzi Abdulla bin Ali bin Nassir kwenye ***Inkishafi*** yake anasema na moyo wake;

Ewe, moyo, enda sijida yake
Hela! Tafadhali unabihike
Shetani Rajimi asikuteke
Kesho kakuona kuwa kamaye...

**Chuku**

Chuku ni usemi wenye kutia chumvi jambo linalozungumzwa. Shaaban Robert katika *Kusadikika* (Uk.25) amesadifu kwa kutia chumvi pale aliposema, "Majuju ni taifa lafi na litishalo kabisa. Kila kitu kigumu kijulikanacho duniani kilikuwa laini kama mkate kati ya meno ya Majuju, na kilicho kichungu kilikuwa kitamu kama asali katika maonjo yao. Kwa ulafi uliokithiri viumbe hawa walikuwa hawajui halali wala haramu..."
(a) Riwaya ya kwanza ya Kiswahili iliyoandikiwa na James Mbotela ina sehemu kubwa na nzuri ya mfano huu wa chuku. Wakati mhusika wake mmoja Juma anasimuliwa hadithi na nyimbo za Mpanda, chumvi ya kutosha inanyunyizwa katika maelezo hayo hasa habari za samaki wavuliwao huko na mihogo ilimwayo. Kuhusu samaki tunaambiwa hivi:

"Samaki wa kwetu wachomwapo, makaa ya moto huzimika kwa ajili ya mafuta mengi ya samaki. Kisha, hapo tuchomapo samaki mmoja, ni lazima tuwaite majirani waje kutusaidia".

Na kuhusu mihogo ilimwayo Mpanda siku hizo yaelezwa hivi,

"... Ukitaka kuula muhogo wa kwetu, muhogo ambao wewe mwenyewe umeupenda, wakati wa kuung'oa ni lazima ualike watu waje wakusaidiye kung'oa. ...Ile mihogo ...ilipong'oka iliwaangusha hao waliokuwa wakiing'oa. Haiwezekani kung'olewa mingi, shina moja hung'olewa asubuhi, na jingine saa za jioni, kwa jinsi ilivyo mikubwa! Ukiona utadhani ni pembe za ndovu. Hao waing'oao, siku ya pili yake huwa na mavune". (Uk. 4)..

*Kurwa na Doto* riwaya iliyoandikwa na Muhammed Farsy imejaa chumvi hapa na pale. Tunu ya mimba na shauku ya harusi, ilikuwa na harakati zake. Mimba iliengwaengwa na kungojewa kwa hamu kubwa. Nikaha ya Faki ikaandaliwa kwa heshima zote uzijuazo. Mwandishi wa riwaya hii anaelezea hadhari kubwa iliyochukuliwa na wenye shughuli hii ili kuifanikisha hasa katika kufuata mila na desturi za Kiswahili za matambiko. Tazama chuku iliyopigwa, "panga (pahala pa tambiko), mizimu, na makaburi yalisemeshwa na kupewa habari ya harusi na mimba, kwa

madhumuni ya kutaka wakuu wa humo wayatilie baraka mambo hayo. Kadhalika palisimamishwa ngoma, pepo wa Kurwa na Mama yake wakapewa ulezi na harusi zao. Majirani, masahibu na wahisani walipewa zawadi mbalimbali" (Uk. 57).

Na saa za kujifungua kwa mzazi zilipokaribia kila hadhari ilichukuliwa hasa katika kuwakusanya wataalamu na wanazuoni wote. Farsy anasema, "Siku zilipokaribia Kurwa alipokuwa na uchungu wa kugeuza, paliitwa waganga na waganguzi, mashehe na masharifu, wakunga na walimu, kumtazama na kumwombea Mungu amsalimu salama" (Uk. 57).

Jahadmy katika *Waimbaji wa Juzi* anasimuliwa jinsi tajiri mmoja wa Kimvita alivyoandaa karamu kubwa kwa kufanikisha arusi na ili kutaka sherehe hiyo itiye for a aliwakodi waimbaji wa taarabu wa Zanzibar akina Siti wa Saadi. Maelezo ya shamrashamra hizo ilikuwa chuku iso doa wala toa. Jahadhmy anasema, "Ikiwa siku kumi na nne walizokaa Mvita ni siku za anasa tupu mji umeingia kishindo cha furaha - watu ni kula tu na kunywa, na kufanywa furja - hapalalwi masiku wala hapaamkwi mchana. Karamu na ngoma zimechacha asiye na mwana aeleke jiwe!" (Uk. ).

Mwimbaji wa taarabu anamwimbie mpenzi wake kuwa pendo lake linathamani ya yakuti ambayo usiku na mchana linang'ara na kuenea chumba kizima hii ni chumvi tosha,

Pendo lako pia yakuti, moyoni limeshakaa.
Mchana na lailati, Nuru yake huzagaa
Ah! Mpe nimo peponi.

Ama kweli Waswahili wamesibu waliposema ukistaajabu ya Musa utayona ya Firauni. Hapa mpenzi anamwaridhia mwenzake kuwa kwa jinsi anavyompenda sana basi roho yake daima milele itaselele kwake.

Zawadi ni roho yangu, Toka leo mali yako
Nakupa kwa radhi yangu, Ili iwe tunzo yako
Madhali wewe ni wangu, *Roho yangu mali yako.*

Na mshairi maarufu wa karne ya 19 Muyaka, anajitapa kwa kusema "anayemkataa, hamrudii tena". Anaelezea kuwa atafanya kila njia mpaka asiwepo moyoni mwake. Yeye anafananisha na jelezi alilonalo. Kama matapishi hayatoki basi atatafuta unyoya wa kanda, msuwaki, tumbaku ya kunusa na kufanya kila mbinu itakayo mfanya atapike. Muyaka anatongoa hivi kishairi na kutia chumvi,

Tapishi lisipokuya, kwa moyo wangu kufunga,
Hujitiami unyoya, unyoya mwema wa kanga,
Na misumari hitia, na matumbaku ya unga,
Sikai ukanongonga, haeri hajitabikia.
(Muyaka: 27)

**Tabaini**

Tabaini ni usemi wenye dhana kya kukinzana lakini maana ya msingi haitenguki. Katika vitendawili viwili hivi kama kiwakilishi halisi cha fasihi simulizi, ukinzano wa dhana moja katika tungo moja unajitokeza. Hebu tuangaliye,

1. Mkubwa *ananiamkua* mdogo *haniamkui*
   (kenda kavu na mbichi)
2. Yeye anatuona sisi *hatumuoni*
   (Mungu)
3. Futi *kafunika* futi *kafunua*
   (Nazi – kumbi, nazi, maji)

Na katika methali za Kiswahili dhana hii imetawaliwa sana. Katika mifano ifuatayo katika pingili ya kwanza ya tindi kitenzi kinajitokeza na katika pingili ya pili ya tindi kitenzi hicho hicho kinatumika lakini kwa kukana kama ilivyokuwa mifano hiyo hapo juu ya kitendawili. Hapa dhana ukinzano inajidhihirisha.

1. Anayetaka *hachoki,* hata akichoka keshapata
2. Mtu *hakatai* wito, hukataa aitwalo

Lakini katika methali hakuna ukinzano wa kitenzi kimoja kutumika kwa kukubali na kukataa tu kama vile hapo juu – hachoki – akichoka, bali upo ukinzano wa maneno yenye kinyume na hiyo pia huleta ukinzano. Kwa mfano:

1. Kukopa harusi, kulipa matanga
2. Mwanzo kokochi, mwisho nazi

Katika methali hizo kuna neno *kukopa* linalofuatiliwa na kulipa na kuna neno harusi linalofuatiliwa na kinyume, *yaani matanga.*

Mshairi maarufu wa Kiswahili Muyaka bin Hajji anachora shairi lenye maneno yenye kukizana katika shairi lake aliloliita "Ujumbe" (Muyaka: Uk.96) na katika beti mbili hizo shairi linasema hivi:

Tumwi anenda senenda, fikilia usifike,
Kisa tenda usitende, furahi wala si teke (sicheke),
Darajani usipande, wala tini (chini) usishuke,
Akitaka usitake, akikubali kataa.

Mjumbe anajibu:

Tumwi hanendi makwenda, mewasili hakufika,
Kisa hatendi matenda, hakufurahi mateka (mecheka),
Hata daraja ya mwanda, pasi la pili meshuka,
Ametaka hakutaka, kukubali mekataa

Riwaya tatu za Kiswahili zilizoandikwa moja na Shaaban Robert na mbili na Muhammed Suleiman zimechota dhana hii ya ukinzano. Kutoka *Kusadikika* (Uk. 30) mwandishi anatuchorea ukinzani:

"Lila na Fila hawatengamani. Kinywa cha Lila kikisema, sikio la Fila hujidai halisikii, jicho la Lila likiona, lile la Fila hujifanya halioni, moyo wa Lila ukijilainisha kwa mapenzi na huruma, ule wa Fila hujifanya mgumu kama jiwe..."

Mwandishi wa *Kiu* (Uk. 46) na wa *Nyota ya Rehema* (uk.133) Muhammed Suleimani anadema hivi katika hizi riwaya mbili tofauti, zenye mazingira tofauti na kutungwa katika nyakati tofauti lakini zinazo fanana kwa mtanzamo wa kimatathali za semi. Kutoka katika *Kiu* imeandikwa hivi:

"Nilimeza mwungwana nikamtema mtumwa"

Na katika *Nyota ya Rehema* muhusika Rehema anajawa na mawazo yanayochorwa hivi:

"Mara kwa upande wa tamaa akiota fanaka, kwa hofu akibashiri"

**Takriri**

Takriri ni usemi unaojidhihirisha katika neno au kifungu cha neno kwenye mfululizo na mfuatano wa sentensi. Hii ni moja ya stadi za kisasaa katika tanzu kadhaa za fasihi ya Kiswahili. Na katka *vitendawili,* haya yanajitokeza hivi:

*Huku fungu huku fungu* katika bahari (Nazi)
Au katika Kitendawili kingine,
Mama kazaa mtoto na mtoto kazaa mtoto na mtoto
Kazaa mtoto (Kuku na yai).

Na hata katika ushairi hali ya kurejearejea hujitokeza kama ilivyo katika nyimbo ifatayo ya taarabu,

*Sema* usiniogope, Wala usione haya
*Sema* usitapetape, Wajumbe kunitumiya
*Sema* na mimi nikupe, Unalolihitajiya

Na katika methali, dhana hiyo pia inajitokeza.

1. *Hayawi hayawi*, huwa
2. *Awali ni awali*, awali mbovu hapana

Riwaya mbili hizi ile ya *Kiu* na *Rosa Mistika* zimetumia tamathali semi hizi katika ujenzi wa riwaya zao. Muhammed Suleiman katika Kiu anachora hivi:
"...Roho *yao moja, moyo wao mmoja*, nia yao *moja* na siri yao *moja*..."
(Uk. 46 - 47).

Kezilahabi katika *Rosa Mistika*,
"*Hawa jamaa walirithi, walirithi hawa jamaa*,
*Walirithi* michungwa na miembe, *Walirithi* migomba yote.
*Walirithi, walirithi... Walirithi* kila kitu ndani ya nyumba.
*Walirithi* paka na mbwa, *Walirithi* majani yaliyokuwa juu ya paa, na miti yote
*Walirithi* paka na mbwa, *Walirithi* majani yaliyokuwa juu ya paa, na miti yote
Iliyofanya nyumba isimame, *Walirithi* mashamba yote. *Walirithi* kuku, walirithi hata mbolea ya ng'ombe. *Walirithi*. Hawa jamaa kweli *walirithi*..." (Uk. 116).

**Simango**

Simango ni usemi wenye kumkebehi au kumtusi muhusika moja kwa moja bila ya kumficha au kumpigia fumbo. Kazi za tamathali hizi zikitolewa panapohusika dhana husibu. Muyaka, mmoja wa washairi maarufu katika upwa wa Afrika ya Mashariki anamtusi mpenzi asiyekuwa na shukurani wala fadhila na yusawa na punda asiyeleta faifa kwa bwana wake. Katika beti tatu zifuatazo anatoa faida ya kufuga ng'ombe kikiwa kama kielelezo tu:

Mfuga hufuga ng'ombe, Kashiba bubu kakama
Na samli lembelembe, Kiwa na haja katuma
Na nyama tindi nisumbe, Niwe katika hishima
Mfuga punda kilema, Hukujambia mashuzi!

Mfuga hufuga nyati mshabaha kama ng'ombe
Samli na ziwa witi na nyama, na juu pembe
Mfuga punda si zumbe! Hukujambia mashuzi

Mfuga hufuga mbuzi nyama mwenyi madhila
Ukawata yako kazi wala pasiwe na ila
Ukenda katika zizi kumtinda na kumla
Mfuga punda, madhila! Hukujambia mashuzi.

Na mshauri mwingine katika kumtusi mpenzi wake alitongoa hivi katika jukwaa la tarahu:

Sasa jamvi la wageni, wajapo huwapokea
Imekutoka thamani, Mtu duni mebakiya
Hata mbwa wa njiani, Kikuona hukimbia.

Kutoka *Nyota ya Rehema* (Uk 48) katika kinywa cha muhusika, simango inatamkwa hivi:

"...Mimi nilimtaka mtu mzima anayejua kulea, si mtoto mdogo asiyemaliza kulelewa...."

Ukichunguza methali nyingi zina hali ya kusimanga na husibu pale zinapotumika. Hizi tatu ni mfano tu:

1. Ganda la muwa la jana chungu kaona kivuno.
2. Jino la pembe si dawa ya pengo
3. Jogoo la shamba haliwiki mjini.

**Kejeli**

Kejeli ni kinyume na ***Simango***. Huu ni usemi ambao maana ya ndani ni kinyume cha yale yasemwayo. Beti mbili hizi za shairi zina kejeli kali kwa mnyonge.

| | |
|---|---|
| Si yake farasi (fakiri) | kweli nakwambia |
| Nguru kwa ugari, | Ameuzoea |
| Ziwa kwa sukari | Kimpa huliya |
| Kimpa huliya, | Akasikitika |
| Dole hujitia, | Akayatapika |
| Jamani uzia | Ulionifika. |

Mfumo wa fedha ulikitwa na ukoloni mkongwe na baadaye kuendelezwa na ukoloni mamboleo, unakejeliwa na mshairi. Kejeli hii inaunganishwa kati ya mfumo wa fedha na tamaa ya fedha yakupenda fedha inayosisitizwa na ibada ya kusali. Wanyakyusa hapa wanawakejeli wazungu jinsi wapendavyo fedha kwa kutumia dini.

Balikalija anasali wapi
Kwenye mawe kwenye mawe
Watemi wanasali wapi
Kwenye mizimu kwenye mizimu

*Wazungu* je wanasali wapi
Kwenye pesa *kwenye* pesa.

Na wimbo mwingine wa kejeli unaopiga fumbo uvivu wa kazi.

Hilo gogo la mgongo
Kwetu twalipiga picha
Lachezewa kifaduro
Haliwekwi uakila
Mnayo, ngoko hiyo mwaiona
Joto juu ya kichwa

Methali nazo zimejisheheneza dhana hiyo ya kejeli kama inavyoonekana mara kwa mara katika tanzu hii.

1. hawi Mussa kwa kuchukiua fimbo
2. Uzuri wa mkakasi ndani kipande cha mti
3. Viovu la kinyesi ni malazi ya bata

Riwaya fupi *Kicheko cha Ushindi* inachangia kejeli pale ilipoandikwa hivi: "hakika Bilisi alifanya jambo kumpa Rajabu shemeji kama yule…" (Uk. 6).

### Misemo

Ni kipengele cha tamathali za semi katika tanzu nyingine. Tuanze kwanza kuchunguza kutoka katika ushairi wa Kiswahili hasa katika beti chache za muziki wa tarabu.

*Kupeana ni kikowa*, Toa na wewe upewe
Mwungwana akipewa, Lazima naye atowe
Kama huwezi kutoa, Vya watu usichukuwe.

Katika riwaya ya *Kiu*, Kiu ya misemo inakakwa pale mwandishi anapotumia misemo miwili mwafaka katika tungo yake kama hivi inavyotiririka:

> "Werevu hujenga na kuimarisha kwa pato hilo, mazungu shetani kwa ngoma na kutia jando kwa kaango na mafisaidi huwachwa wake wabaya eti kuoa wazuri ambao katika vuno la mwakani watarejea unaya vilevile…" (Uk. 89).

### Tafsida

Tafsida au wengine huita tauria ni tamathali ya usemi ambayo inajaribu sana kukwepa karaha au uchafu ili kuwezesha hata matusi kutamkwa hadharani. Kunga hii ya semi ikitumiwa katika kazi za fasihi hujenga itifaki nzuri. Waswahili katika mazungumzo yao

ya kila siku na hasa katika shughuli zao za mila na desturi na katika maisha ya kila siku, misemo kadhaa wa kadha ya Kiswahili hutumia kunga hii ya tafsida. Misemo ifatayo inaficha kwa kiasi kikubwa karaha au hofu Fulani iliyofichwa. Kwa mfano Waswahili husema,

i. Kuchungulia kaburi (kuwa mahututi, kukaribia kufa)
ii. Ana macho ya nje
iii. Kujifungua (kuzaa mtoto)

Katika *Rosa Mistika,* riwaya iliyoandikwa na E. Kezilahabi yanachorwa mazingira ya tafsida ambayo yanaficha matusi bila kutamka wazi wazi. Kezilahabi anatueleza hivi juu ya Flora alipokwenda kuoga.

> "Flora akienda kuoga, hujiangalia angalia kwa muda mrefu kabla ya kuoga. Hutazama matiti yake ambayo sasa yanaanza kuwa makubwa, hujipapasapapasa kwa mikono kutoka mgongoni mpaka pale matako yanapotelemkia" (Uk. 4).

Farsy na riwaya ya *Kurwa na Doto* anatumia lugha ya murua anapoelezea kukua kwa Kurwa. Farsy alisema,

> "*Alipovunja ungo* alikataa kuwa mwali wa mfereji, alikakawana na kumrai mama yake amkoshe kwa mambo na uzia, yaani amtie unyagoni". (Uk. 12)

Misemo "bao la mkahawani" na chano cha mji" ni matusi makubwa kwa mwanamke ikimaanisha umalaya uliokithiri. Katika *Utengano* Said Ahmed Muhammed anatumia misemo hiyo katika kumwelezea tabia mbaya hiyo ya muhusika wake mmoja Maimuna. Muhusika Kijakazi akiwa na muhusika mwenzake, Shoka, anamsusuika Maimuna kwa tamko, hili, "Shoti anavyoringa, utafikiri si bao la mkahawani, Nani naye anayeshtua watu, alitupiwa mbwa hamtaki" (Uk. 139).

Naye Maimuna katika kujibu sengenyo hizo katika starehe zao za pombe alisema:

> "Toka lini mtu wa vilabuni kuwa na mtu mmoja? *Si chano cha mji tu?* Kila mtu hukifulia" (Uk. 142) (Msisitizo wangu).

## Taashira

Taashira ni tamathali inayohusisha kwa kiasi kikubwa uhusiano wa kitu na kichukuzi chake au kitu na chanzo chake ama chanzo na kinachotolewa. Baada ya kutaja waziwazi wakati mwingine hutumi tamathali hii ya taashira. Kwa mfano katika mazungumzo ya kawaida mtu huwezi akamwambia mwenzake kuwa, "sufuria yako inachemka" hapa kwakweli kinachochemka sio sufuria bali kile bali kile kilichomo ndani ya sufuria. Ama mtu anaweza kumwambia mwanawe "usikae mvuani" hapa mtu hawezi kukaa mvuani bali ni matokeo ya mvua ndio yatakayomuathiri. Wakati mwingine watu husema, "nyuma

nzima ilikwenda mpirani". Ukweli ni kwamba haiwezekani nyumba kutembea hadi mpirani lakini wale watu wanaoishi ndani ya nyumba ndio hasa waliokwenda mpirani.

Na katika nyimbo ifuatayo ya tarabu inazungumzia kiberiti na petroli kuwa ni vitu vya hatari kuviweka pamoja. Ukweli mwimbaji anaongelea sio kibiriti na petroli vitu ambavyo kila mmoja anavijua bali anaongelea juu ya kumweka msichana na mvulana pamoja. Beti mbili hizi zinaonyesha mfano huo:

Kibiriti na petroli  Iwapo umeviweka
Hivi ni vitu viwili  Visije kukutanika
Kusalimika muhali  Lazima patalipuka
Bora uvitenge mbali  hapo utasalimika
Katu haiwi salama  Jambo hili ni hakika
Moto kuja ni lazima  Na wala hapana shaka
Tena taabu kuuzima  Moto ukisha kuwaka
Moto wake ni nakama  Lazima kuhasirika

Mwimbaji mmoja maarufu kisiwani Pemba alitongoa wimbo wake unaotukuza kilimo ingawa wenyewe alikuwa anazungumzia juu ya pembe kama mumewe. Mwanamama huyo akimsusuika mumewe alitongoa:

Ukinipenda usinipende
Nina mume wangu jembe

Kutoka riwaya ya *Kiu* mwandishi anaonyesha jinsi kichukuzi kinavyoathiri kinachochukuliwa kwa maana ya kuwa jinsi jua linavyoweza kuathiri chakula. Ingawa kilichotajwa ni sahihi si chakula.

"*....miongo* ingekuwapo na kuathiri *sahani"* (Uk. 58)

Na katika methali ya Kiswahili msemo ufuatao unatumia kumbi na kiti lakini vifaa hivi vinawakilisha tu madaraka kwa mwenye kiti na kumbi ni kwa mtu lofa. "Aliyekupa wewe kiti ndiye aliyenipa mimi kumbi"

**Nasiha**

Nasiha ni tamko lililojaa nasaha na busara. Nyingi ya nasiha ni methali za kiswahili zinazotumika kila siku katika maisha ya kawaida ya kutoa nasaha. Wakati mwingine hata beti za mashairi husimama kama nasiha. Aidha katika riwaya za Kiswahili huweko sentensi fupi fupi zenye kubeba tamathali hii. Kwa mfano Mohammed Said Abdulla na riwaya yake *Mzimu wa Watu wa Kale* anafafanua dhana ya elimu na umuhimu wake kwa kutumia dhana ya mwangaza na shida impatayo mtu aliyesoma. Naye anasema hivi:

"...ukitaka kujua asili ya mwangaza ingia kizani" au "ukitaka kujua raha ya mtu aliyesoma, tazama tabu ya mtu asiyesoma",...(Uk. 3)

Naye Shaaban Robert staidi wa mashairi ametutongolea beti mbili hizo tofauti zenye kuonyesha nasiha kamili. Kutoka kitabu cha Insha na Mashairi

Penzi la kujitolea
Ndilo penzi la daima
Twapata kwa kuzaliwa
Na atupaye ni mama
Hatupati kwa ulua
Aidha ushairi wa beti nyingine unasema hivi,
"Chacha huzaa moto
Moto huanza kijito
Tone bahari na ziwa"

Methali za Kiswahili nyingi zina sifa za nasiha. Ifatayo ni mifano michache tu

1. Ving'aravyo vyote si dhahabu.
2. Ukitaka kuruka agana na nyonga.
3. Mwenda pole haumii mguu.
4. Usiku ni libasi bora.

**Ritifaa**

Ni tamathali ya usemi kitu kisicho uhai huwa kinasemeshwa au vile mauti huombolezwa na kuliliwa na kite na kwikwi au kusifiwa kama vile nafsi yake ingali hai. Aidha vitu vya kufikirika na ambavyo duniani hivi sasa haviko husimuliwa kama vile viumbe katika hali halisi ya maisha vipo.

Tunza ushairi ndiyo inayotawala kwa kina na maki kubwa tanzu hii. Washairi waliowengi wanaonekana kuongea ana kwa ana na watu mashughuri waliokufa katika nyakati mbalimbali.

Euphrase Kezilahabi na Kichomi chake anazungumza na washairi maarufu miongoni mwao ni marehemu Mnyampala, Amri Abeid na Shaaban Robert. Yeye anawaambia hivi:

Habari gani? Mnyampala Mbukwa! Mimi
Ni K. bin T unafurahiaje maisha baada ya kufa
Wasemaje malenga wetu. Mwambiye Robert
Kwamba yule mzungu amefanya kazi nzuri
Na kwamba siku hizi Waafrika wenyewe
Wameanza kuipalilia bustani yake. Mwambiye

Kaluta kwamba ule mzozo sasa unajulikana
Na kwamba watu wengi siku hizi hutunga mashairi.
(Uk. 41)

Mulokozi na Kahigi katika *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu* wanaongea na marehemu Mao Tse Tung kwa lugha ya maombolezo. Sehemu ya beti hizo waimba hivi:

Hebu nikuimbie wimbo wa mwisho Mao
Wimbo wenye kubomoa ulichokibomoa na kuimarisha ulichokiimarisha
Kwa nguvu mpya ya sanaa mpya iliyonaswa
Katika mivukuto ya enzi zetu
Japo hutaki niruhusu nikusifu nakukumbuka
Maana umeacha katika Uchina
Maua mekundu yamechanua
Na katika nchi yangu pia
Maua mekundu yatachanua ...(Uk. 114)

Mshairi maarufu wa Kiswahili Marehemu Shaaban Robert wakati wa uhai wake anaongea na marehemu mkewe, Bibi Amina:

Amina umejitenga, kufa umetangulia
Kama ua umefunga, baada ya kuchanua
Nakuombea mwanga, poponi kukubaliwa
Mapenzi tuliyofunga, hapana wa kufungua

Nilitaka unyanyuke kwa kukuombea dua
Sikupenda ushindike maradhi kukuchua
Ila kwa rehema yake Mungu amekuchagua
Mapenzi tuliyoyafunga hapana wa kufungua.

**Tanakali ya Sauti**

Huu ni usemi unaojitokeza katika kazi kadhaa za fasihi za fasihi. Muhammed Suleiman katika riwaya yake fupi ya *Kicheko cha Ushindi* unaonyesha jinsi maneno ya lugha yanavyo weza kuiga sauti halisi sauti ya mapigo ya saa na vishindo vya miguu vinaelezwa hivi:

"...*Cha! Cha! Cha!* alisikia saa mithili ya miguu ya paa katika mbuga za majani makavu. *Ti! Ti! Ti!* moyo nao ulifukuzia...."

Katika riwaya ya Mzimu wa Watu wa Kale mwandishi akikazia weusi wa

Msa alisema, "Bwana Msa alikuwa kijana Mwafrika ambaye alikuwa mweusi tititi na mtu akiulizwa "Bwana Msa gani? Hujibu si yule mweusi yahe!

Moja ya kasida maarufu ya kusifu wajihi wa Nabii Muhammed inatumia tamathali ya usemi huu, moja ya mistari ya ushairi huo unasema hivi:

Rangi yake ni mweupe    Ila si mweupe *pepe!*
Alikuwa na weupe    Wenye wekundu haiba

Na huku mwimbaji wa tarabu katika kuisifu zambarau kwa ladha na umbo lake pia anaeleza rangi yake nyeusi illivyokua na kusomaa. Ustadhi anaimba hivi huku akiwekea uzito wa "tanakali sauti".

Ikiwa juu ya mti    Ni nini utailiza
Iwe nyeusi tititi    Utasema imeioza
Uipate kwa bahati    Mwili itakuregeza

**Hitimisho**

Kwa haya machache yaliyojitokeza, imedhihirika kuwa lugha ya Kiswahili sio lofa au fukara katika tamathali za semi. Wale wanaochamba lugha hii kuwa eti ni kiwete na haiwezi kufuata mdundo na midenguo ya maendeleo ya jamii au haiwezi kwenda kwa kutia ngosho na fani za siku hizi za kisiasa; kiuchumi au kisayansi, hazina hii inajidhihirisha kujikimu na kujitosheleza yenyewe. Na kama utazuka ubishi wa lugha kuhusiana na kuweza kujikimu na kujiruzuku katika nyanja za fasihi, mifano hii michache inaweza kuwakebehi na kuwasuta bila kimeme na maya wale wote wanaodhani au kushahidia kuwa lugha hii ni pungufu kwa fani hiyo.

Zaidi ya hayo kisionekane kiroja kuwa labda tamathali zinazojitokeza katika Kiswahili na hasa fani ya fasihi kuwa eti ni ya kipekee. Ichimbe lugha yoyote duniani katika mwelekeo huu wa fasihi lazima ukipiga mbizi ukiibuka utakuja na "lulu" hizi za tamathali za usemi ukiwa umezifumbata katika viganja vyako. Macho yatakodolewa, moyo utafurahika na mikono itatetemeka kwa furaha ya mavuno mazuri ya sanaa katika lugha! Hivyo yale yapatikanayo katika lugha ya Kiswahili na hasa kama hili nililojaribu kulidhihirisha hujitokeza katika lugha inayoishi duniani. Kiswahili ikiwa moja ya lugha hizo haijibagui au kujitenga na ukweli huo. Moyo wa mswahili gani utaosita kupiga mapigo yake ya moyo kwa haraka kwa furaha unapothibitishwa kuwa Kiswahili si "mkembe" bali "nyakanga" aliyebobea katika mizungu ya huku ya kujaaliwa na tamathali za semi teletele!